**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA TARIME**

***Unapojibu tafadhali taja:***

**Kumb. Na. HWT**/E4/2/83 04.10.2021

# *TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI*

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Tarime amepokea kibali cha Ajira mbadala kutoka kwa Katibu Mkuu Utumishi chenye **Kumb.Na.FA.170/377/01"B"/84** cha tarehe **10.09.2021** kwa ajili ya kuajiri **Watendaji wa Vijiji Daraja la III** nafasi **8** pamoja na **Dereva** nafasi **1.**

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Tarime anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi wazi za kazi zilizoainishwa katika tangazo hili, kama ifuatavyo:

## 1.0 MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA LA III NAFASI (8)

### 1.1 MAJUKUMU YA KAZI

i. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.

ii. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na mali zao,kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.

iii. Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa Mipango ya maendeleo ya kijiji.

iv. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.

v. Kutafsiri na kusimamia sera,sheria na taratibu.

vi. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa,umaskini na kuongeza uzalishaji mali.

vii. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya kitaalamu katika kijiji.

viii. Kusimamia,kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za kijiji.

## 1.2 SIFA ZA MWOMBAJI

i. Awe Mtanzania.

ii. Awe na Elimu ya Kidato cha Nne au cha Sita.

iii. Awe amehitimu mafunzo ya Astashahada (cheti) katika moja ya fani za Utawala, Sheria, Maendeleo ya Jamii, Elimu ya Jamii na Sayansi ya Sanaa,Usimamizi wa Fedha, kutoka chuo cha Serikali za Mitaa cha Hombolo –Dodoma au chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

*iv.* Awe na umri wa **miaka 18** au zaidi na asiwe na *umri unaozidi miaka 45.*

v. Awe na afya njema,mchapa kazi na mwenye utayari wa kufanya kazi mahali popote katika vijiji vya Halmashauri ya Wilaya ya Tarime.

vi. Unatakiwa kuwa na namba ya utambulisho wa Uraia kutoka mamlaka ya vitambulisho vya Taifa **(NIDA).**

## 2.0 DEREVA DARAJA LA III NAFASI (1)

## 2.1 MAJUKUMU YA KAZI

i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.

ii. Kuwapeleka Watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.

iii. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari.

iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali.

v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftali la safari.

vi. Kufanya usafi wa gari na

vii. Kufanya kazi nyingine kadili utakavyoelekezwa na msimamizi wako.

## 2.2 SIFA ZA MWOMBAJI

i. Awe Mtanzania.

ii. Awe na Elimu ya Kidato cha Nne na lessen ya daraja E au C1 ya uendeshaji magari mwenye uzoefu wa kuendesha magari kwa muda usiopungua miaka mitano (5) bila kusababisha ajari.

iii. Awe na cheti cha majaribio ya ufundi daraja la II au sifa nyingine inayolingana nayo kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali.

*iv.* Awe na umri wa **miaka 18** au zaidi na asiwe na *umri unaozidi miaka 45.*

v. Awe na afya njema,mchapa kazi na mwenye utayari wa kufanya kazi.

vi.

vii. Unatakiwa kuwa na namba ya utambulisho wa Uraia kutoka mamlaka ya vitambulisho vya Taifa **(NIDA).**

**3.0 UTARATIBU WA KUOMBA**

a. Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, Kijiji Cha Nyamwaga, Barabara ya Nyamwaga, S.L.P 16, Tarime-Mara, Simu +25528-2690518, Nukushi: +25528-2690144, Barua pepe: ded@tarimedc.go.tz,Tovuti:www.tarimedc.go.tz

b. Maombi yote yatumwe na nakala za vyeti vya taaluma na vya mafunzo na vyeti vya kuzaliwa vilivyothibitishwa na mahakama au na mtu yeyote aliyeidhinishwa na Serikali.

c. **Testimonials' 'Provisional Results', Statement of Results;** Hati za matokeo ya kidato cha nne na sita **HAVITAMBULIKI.**

d. Waombaji wote waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe kuwa vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika ya **TCU** na **NECTA**

**4.0** Watumishi wote waliowahi kufanya kazi katika Utumishi wa Umma wakaacha,wakastaafu,wakastaafishwa au wakafukuzwa hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.

**5.0** Vyeti vyote vitafanyiwa uhakiki kwa kushirikiana na mamlaka husika za **NECTA, TCU** na Vyuo waombaji walivyosomea na endapo itagundulika mwombaji amehusisha vyeti vya kughushi kwenye maombi yake atachukuliwa hatua za kisheria.

**6.0** Mshahara utalipwa kwa kuzingatia ngazi za mishahara ya Serikali **TGS 'B'**

7. ***MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI***

Maombi yatapokelewa katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya ya Tarime katika kipindi cha **siku 14 (muda wa kazi)** kuanzia tarehe ya tangazo hili na mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **18.10.2021** saa **9:30** alasiri.

8. Tunawakaribisha wote wenye sifa zilizotajwa hapo juu kuwasilisha maombi yao kwa utaratibu ulioelekezwa.

*Frederick D. Mallya*
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**<u>TARIME</u>**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA TARIME